MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU-SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU; MHESHIMIWA JENISTA J. MUHAGAMA (MB) KWENYE MAADHIMISHO YA KILELE CHA MBIO ZA MWENGE WA UHURU, KUMBUKUMBU YA KIFO CHA BABA WA TAIFA NA WIKI YA VIJANA KITAIFA MKOANI SIMIYU TAREHE 14 OKT0BA, 2016

- **Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;**
- **Mheshimiwa Moudline Cyrus Castico, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto – Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;**
- **Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi, Zanzibar,**
- **Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu;**
- **Waheshimiwa Anthony Mavunde na Dkt. Abdallah Possi, Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu;**
- **Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa Simiyu;**
- **Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria;**
- **Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;**
- **Waheshimiwa Wawakilishi wa Madhehebu mbalimbali ya Dini;**
- **Waheshimiwa Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa;**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama mbalimbali vya Siasa;**
- **Waandishi wa Habari;**

- **Ndugu Wananchi;**
- **Mabibi na Mabwana.**

Mheshimiwa Rais,
Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, kumbukumbu ya kifo cha baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Wiki ya Vijana Kitaifa kwa mwaka 2016 Mkoani Simiyu. Najua unayo majukumu mengi ya Kitaifa na Kimataifa, lakini kwa kuthamini shughuli hii umeamua kuja kuungana nasi leo hii, **Tunakushukuru sana.**

Pia napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Anthony Mtaka Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, viongozi na wananchi wa Mkoa wa Simiyu kwa kukubali kuwa wenyeji wa maadhimisho haya ya kitaifa lakini pia kwa maandalizi mazuri ya shughuli hii. **Nasema ahsanteni sana.**

Aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa Moudline Cyrus Castico, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto – Serikali ya Mapinduzi Zanzibar**,** watumishi wa Wizara yake na Watumishi wenzangu kutoka ofisi ya Waziri Mkuu, kwa ushirikiano mzuri waliouonyesha katika kuandaa, kuratibu na kusimamia shughuli hii kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Rais;
Kabla sijaendelea naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na

wewe Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar baada ya uchaguzi Mkuu wa mwaka jana 2015, **Ninawapongeza sana.** Sote kwa pomoja tunaunga mkono jitihada mbalimbali mnazozichukua kwa lengo la kuboresha ustawi wa wananchi wetu na Taifa la Tanzania. Tunakuahidi kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili tuweze kufikia malengo tuliyoyakusudia kama Taifa. Tutaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na kuliombea Taifa letu Amani na Utulivu kwa watu wake ili mtuongoze katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Rais;

Naomba sasa nichukue nafasi hii kwa ruksa yako Mheshimiwa Rais kutambua na kuthamini mchango wa hali na mali wa wadau wetu wa shughuli za Mwenge wa Uhuru na maendeleo ya Vijana kwa ujumla waliochangia katika kufanikisha maadhimisho haya ya Kitaifa hapa Simiyu***.***

Baadhi ya Wadau hao ni:

(i) Benki ya NBC
(ii) Benki ya NMB
(iii) Shirika la Umoja wa Mataifa Tanzania
(iv) Restless Development Tanzania
(v) PSI Tanzania
(vi) SSRA
(vii) Under The same Sun
(viii) Standing Voice
(ix) Asasi za Watu wenye Ulemavu Nchini.

Mheshimiwa Rais;

Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizinduliwa rasmi Mkoani Morogoro tarehe 18 April, 2016 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya uzinduzi huo, Mwenge wa Uhuru umekimbizwa katika Halmashauri na Manispaa 179 ndani ya Mikoa yote 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa siku 179 na leo Mbio hizi zinafikia kilele chake hapa Mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Rais;

Kama tunavyofahamu sote Mwenge wa Uhuru ni ishara ya Uhuru wa nchi yetu ya Tanzania na chombo muhimu cha kujenga undugu, umoja, mshikamano na kudumisha amani katika nchi yetu. Chombo hiki pia, kinatumika kumulika vitendo vya dhuluma, rushwa, ufisadi na unyanyasaji wa wananchi. Vile vile Mbio za Mwenge wa Uhuru zimekuwa ni kichocheo cha maendeleo ya wananchi, ambao kupitia Mbio hizi wamekuwa wakihamasika na kushiriki katika kubuni, kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yao kwa kushirikiana na Serikali. Miradi hii ndiyo inayowekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru. Hamasa hii inadhihirishwa na ongezeko la miradi inayozinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi kila mwaka kupitia Mbio hizi. Kwa mfano:-

- Mwaka 2015, jumla, miradi **1,342** yenye thamani ya **Tshs. Bilioni 463.5** iliwekewa mawe ya msingi na mingine kuzinduliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.
- Mwaka huu wa 2016, jumla miradi **1,387** yenye thamani ya **Tshs. Bilioni 498.8** imewekewa mawe ya msingi na mingine kuzinduliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Thamani ya miradi hii imeongezeka kwa asilimia **7.6** kati ya mwaka 2015 na 2016.

Mheshimiwa Rais;

Kwa kawaida Mbio za Mwenge wa Uhuru huambatana na ujumbe maalum kuhusu masuala muhimu ya Kitaifa na Kimataifa. Hivyo, Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 ulizingatia kauli mbiu isemayo:- "**Vijana ni Nguvu kazi ya Taifa**; "**Washirikishwe na Wawezeshwe**" Aidha, ujumbe wa kudumu uliohusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa **UKIMWI, Malaria, matumizi ya Dawa za Kulevya** na **Rushwa** uliendelea kutolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Rais,

Ujumbe huu umekuwa ni chachu ya kutekeleza jitihada za Serikali za kuwataka Vijana kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili waweze kuondokana na umasikini kwa kujiajiri na kuajiri vijana wenzao. Ili kufanikisha azma hii, Serikali imeagiza Mikoa na wilaya zote nchini kuwatengea vijana maeneo ya kufanyia kazi na kuwawezesha mitaji kupitia asilimia tano za mapato ya ndani ya Halmashauri zao. Tathmini iliyofanywa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, inaonyesha kuwa Jumla ya ekari elfu **84.8** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo na huduma za jamii kote nchini. Aidha, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya **Tshs. Billioni 4.5** zilitengwa na kutolewa kwa vikundi vya vijana kama mikopo ya kuanzisha miradi endelevu ya uzalishaji. Mikoa sita (6) iliyofanya vizuri katika kuhakikisha nguvu kazi hii ya Vijana inatumika ipasavyo kama Serikali ilivyoelekeza. Mikoa hiyo ni:- **Njombe**, **Mwanza**, **Ruvuma**, **Mbeya, Mtwara** na **Simiyu**. Tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili Mikoa yote nchini isimamie kikamilifu agizo la Serikali la kuhakikisha vijana wote nchini wanafanya kazi lakini pia wanawezeshwa.

Mheshimiwa Rais,

Mwenge wa Uhuru mwaka huu umebaini ubadhilifu na udanganyifu katika miradi ya maendeleo na miradi ya vijana katika Halmashauri saba nchini. Udanganyifu huu ni pamoja na baadhi ya miradi kutokidhi viwango na matumizi ya fedha zinazotengwa kama 5% ya mapato ya ndani ya halmashauri kutotolewa kwa walengwa ambao ni Vijana. Watendaji wote waliohusika na udanganyifu huo wamesimamishwa kazi na uchunguzi dhidi ya vitendo hivi unaendelea. Aidha, hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na taratibu za Utumishi wa Umma zitachukuliwa kwa wale wataobainika kuwa chanzo cha udanganyifu huo.

Mheshimiwa Rais;

Kama ilivyo kawaida, kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kilitanguliwa na Wiki ya Vijana Kitaifa. Wiki hii huwapa vijana fursa ya kufahamu na kuenzi mchango wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika harakati za ukombozi wa Taifa hili na jitihada zake za kuleta amani, upendo, mshikamano na uzalendo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Rais,

Maonyesho ya Wiki ya Vijana uliyoyatembelea leo asubuhi ni ushahidi tosha kuwa, vijana wakijitambua, wakipewa nafasi na kuwezeshwa wanaweza kutupeleka kwa haraka sana katika uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Rais,

Wewe mwenyewe umeshuhudia Vijana wabunifu waliobainishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Vijana hawa wamekwisha kutambulishwa kwenye Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusika ili wasimamiwe na kuongozwa kwa lengo la kuendeleza ubunifu wao. Ofisi ya Waziri Mkuu itashirikiana na taasisi hizo kuchangia gharama za kuwajengea uwezo zaidi. Tunajua tukifanya hivyo hawa vijana wataweza kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya sayansi na teknolojia nchini Tanzania.

Mheshimiwa Rais;

Tanzania ikiwa ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, tumetumia Wiki hii kuadhimisha siku ya Vijana Duniani Kitaifa hapa Mkoani Simiyu. Ujumbe wa Siku ya Vijana Duniani kwa mwaka huu ni:- **" Kuelekea 2030: Tokomeza Umasikini kwa uzalishaji endelevu na matumizi yenye Tija".**

Mheshimiwa Rais,

Sisi kama Taifa tumeitumia wiki hii kutafakari na kubadilishana mawazo juu ya uzalishaji endelevu na matumizi yenye tija. Aidha, tumeelezana juu ya mipango ya Serikali ya Awamu ya tano ya kuwa na matumizi yenye tija, kupambana na rushwa, kulipa kodi, na kujenga miundo mbinu itakayosaidia kuleta mageuzi ya uchumi wa viwanda kama njia stahiki ya kuongeza ajira kwa Vijana wetu. Vile vile, Vijana wamejadili nafasi yao katika kuleta mapinduzi haya na kuandaa maazimio ambayo nitayawakilisha Serikalini kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Rais,

Napenda kukufahamamisha pia, kwamba katika Wiki hii ya Vijana tumeweza kuzindua rasmi kampeni ya mapambano dhidi ya ukatili na unyanyapaa wa watu wenye ualbino. Kampeni hii itaendelezwa na Vijana katika mikoa 11 ambayo ni

Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Katavi, Tabora, Singida, Mara, Kagera, Mbeya, Rukwa, na Kigoma kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa hiyo. Watu wenye ualbino wanayo haki ya kuisho, ni wajibu wetu sote kuwalinda.

Mheshimiwa Rais;

Wakati wa Maadhimisho ya Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Waziri mwenye dhamana hutaja Mkoa mwenyeji wa Uzinduzi na Kilele cha Mwenge wa Uhuru kwa mwaka unaofuata. Hivyo, kwa mwaka ujao wa 2017 uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru utafanyika Mkoani ***Katavi*** wakati maadhimisho ya Kilele cha Mbio hizo yatafanyika Mkoa ***Mjini Magharibi- Zanzibar.*** Naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Mikoa niliyoitaja kwa kukubali kubeba jukumu hili kubwa la Kitaifa, nawatakia kila la kheri katika maandalizi.

Mheshimiwa Rais;

Sasa naomba nichukue nafasi hii nikutambulishe kwa Vijana Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ambao leo wamekamilisha kazi waliyotumwa na Taifa kwa siku 179. Aidha, nitakuomba uwakabidhi Hati maalum ya kutambua kazi kubwa waliyoifanya na baada ya kukabidhiwa Hati hizo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru atakukabidhi Mwenge wa Uhuru na baadaye kukusomea na kukukabidhi Risala ya Utii kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2016 ni:-

1. James Sadick Munguji - Kutoka Mkoa wa Simiyu
2. Lucia Vitalis Kamafa - Kutoka Mkoa wa Manyara
3. Alex Christopher Kayuni - Kutoka Mkoa wa Morogoro

4. Munira Said Abassi - Kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi

5. Nahoda Makame Nahoda - Kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba

6. George Jackson Mbijima - Kutoka Mkoa wa Mbeya **(Kiongozi)**

Mheshimiwa Rais;

Kila mwaka kunakuwa na mashindano ya Mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo washindi wa Kanda na Kitaifa hupewa zawadi na Hati mbalimbali. Aidha, Mikoa mwenyeji wa Uzinduzi na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru nayo hupewa Kikombe na Hati maalum. Vile vile, Wadau na Mashirika yaliyochangia kufanikisha shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru nao hupewa Hati maalum.

Mheshimiwa Rais,

Mwaka huu tutaitambua na kuipa Hati maalum Mikoa iliyofanya vizuri katika kutekeleza maagizo ya Serikali ya kuwawezesha Vijana kiuchumi na kuibua fursa mpya za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Rais;

Kwa heshima na taadhima, sasa naomba uniruhusu nitaje tu makundi mbalimbali yatakayopewa zawadi na Hati maalum. Makundi nitakayoyataja yatakabidhiwa Hati hizo na zawadi kwa utaratibu maalum hapo baadaye.

Makundi hayo ni:

1. Mkoa mwenyeji wa Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru ulikuwa Mkoa wa Morogoro; Watapewa kikombe na cheti.
2. Mkoa mwenyeji wa Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Kumbukumbu ya Kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Wiki ya Vijana Kitaifa ni Mkoa wa Simiyu; Watapewa kikombe na cheti.
3. **Mshindi wa Kanda ya I** – yenye Mikoa ya Mwanza, Dar Es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Geita na Songwe ni **Manispaa ya Moshi** kutoka Mkoa wa **Kilimanjaro**; watapewa kikombe, cheti na fedha taslim shilingi 1,000,000/=
4. **Mshindi wa Kanda ya II -** yenye Mikoa ya Tanga, Morogoro, Tabora, Iringa, Njombe, Simiyu na Shinyanga ni **Manispaa ya Iringa** kutoka Mkoa wa **Iringa**; watapewa kikombe, cheti na fedha shilingi 1,000,000/=
5. **Mshindi wa Kanda ya III -** yenye Mikoa ya Ruvuma, Singida, Dodoma, Manyara, Kagera na Mara ni **Wilaya ya Nyasa** kutoka Mkoa wa **Ruvuma;** watapewa kikombe, cheti na fedha shilingi 1,000,000/=
6. **Mshindi wa Kanda ya IV** – yenye Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Kigoma, Katavi na Rukwa ni **Manispaa ya Lindi** kutoka Mkoa wa **Lindi**; watapewa kikombe, cheti na fedha shilingi 1,000,000/=
7. **Mshindi wa Kanda ya V -** yenye Mikoa ya Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi ni wilaya ya **Magharibi 'B'** kutoka Mkoa wa **Mjini Magharibi;** watapewa kikombe, cheti na fedha shilingi 1,000,000/=
8. **Mheshimiwa Rais;**

   Naomba nitaje mshindi wa Kitaifa wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 ambaye ni **Halmashauri ya Wilaya ya Lindi** kutoka Mkoa wa **Lindi** Kanda ya **IV ;** watapewa kikombe, cheti na fedha taslimu shilingi 5,000,000/=

9. Baadhi ya Wadau wa taasisi zilizochangia shughuli za Mwenge wa Uhuru ambao wote watapewa cheti ni:-

   (i) Benki ya NBC (ii) Benki ya NMB (iii) Shirika la Umoja wa Mataifa Tanzania (iv) Restless Development Tanzania

10. Mikoa iliyofanya vizuri katika kutekeleza maagizo ya Serikali ambayo yote itapewa cheti maalum ni kama ifuatavyo:

    (i) Njombe (ii) Mwanza (iii) Ruvuma (iv) Mbeya (iv) Mtwara (v) Simiyu

Mwisho.